

Mkataba wa Ushiriki

Masharti haya yanabainisha sheria na masharti yenye mamlaka kisheria yanayodhibiti ushiriki wako katika mradi wa FreshWater Watch (Kuanzia sasa, "**Mradi**"). Mradi huu umepangwa na kuendeshwa na Conservation Education and Research Trust -Ushirika wa Elimu ya Uhifadhi na Utafiti- (jina la kazi: Earthwatch Institute (Uropa) (kuanzia sasa "**Kampuni**", "**Sisi**") au mojawapo wa **washiriki wetu katika mradi** nyanjani. Iwapo una umri wa chini ya miaka 18, mtu mzima sharti asome na kutia saina mkataba huu.

Maelezo ya Dhima:

Zaidi ya taarifa na sheria na masharti yoyote ambayo huenda umetumiwa kuhusiana na tukio fulani, shughuli zinazotekelezwa zina hatari fulani. Earthwatch na/au washiriki wetu nyanjani wamechukua hatua madhubuti kupunguza makali ya hatari hizi kwa washiriki. Hatua hizi zinaweza kujumuisha (ila hazijikiti tu kwa) kufanya tathmini ya hatari, mipango ya kudhibiti matukio, na kutoa mafunzo na maelekezo ya kutumia vifaa. Ni muhimu kwa washiriki kufuata maagizo ya usalama yaliyotolewa (na maafisa nyanjani, maelekezo yanayoandamana na vifaa au kwenye mtandao), na wawe na mienendo inayopunguza utukiaji wa hatari kwao, na kwa watu wengine katika mradi.

Huenda ukahusika katika mradi kwa njia tofauti, ikiwemo kukusanya data ya utafiti, kushiriki katika programu ya siku moja ya kutoa mafunzo, kuwa sehemu ya wanaotoa mafunzo ya kiutendaji ya mbinu za utafiti, na/au kukusanya data kwa wakati wako kama shughuli ya utafiti wa kujiongoza bila usimamizi wa moja kwa moja wa Earthwatch au mtu mwingine yeyote. Earthwatch (au mshiriki wako nyanjani) huenda akakupa vifaa vya kukusanyia data. Ni wajibu wako kusoma na kuelewa maagizo yaliyoko kwenye kifaa kabla ya kukitumia (kwa kuwa wewe pekee unawajibikia kifaa na matumizi yake). Iwapo una maswali yoyote kuhusu jinsi ya kutumia kifaa au kutekeleza majukumu yako tafadhali wasiliana na Earthwatch (au mshiriki wa mradi nyanjani).

Mradi huu unahusisha hatari ndogo ya kiasili na hatari nyinginezo katika ukusanyaji wa sampuli. Hatari hizo zinajumuisha (ila hazijikiti tu kwa) zile zinazohusishwa na kuwa nyanjani na karibu na maeneo yanamopatakina maji kama vile kukumbana na wanyama pori, mimea yenye sumu, hali kali ya hewa na mandhari yanayotoa changamoto. Kwa kutia saina mkataba huu, unaelewa kuwa hatari kama hizi zinaweza, japo katika hali nadra sana, kusababisha kifo, majeraha, magonjwa, au ulemavu, na unakubali kuwajibikia hatari zinazotokana na shughuli zako zinazohusiana na mradi iwapo zimetajwa humu au la. Wakati unapofanya kazi bila usimamizi wa Earthwatch au mshiriki wa mradi nyanjani, sharti uweze kubainisha iwapo shughuli zako na matendo yako yana maana na yanafaa. Una wajibu wa kufanya maamuzi kuhusu usalama wako na iwapo hali zinazozingira shughuli husika ni salama.

Kwa walio na umri wa chini ya miaka 18 au watu wazima wanaohitaji usimamizi sharti waandamane na mzazi/mlezi ambaye anawajibikia kikamilifu afya yao, usalama na ustawi wao kila wakati, na ambaye amesoma na kutia saina mkataba huu na maelekezo ya usalama yaliyotolewa.

Kwa kujiunga na mradi wa FreshWater Watch, unakubali daima kuwachilia, kutodai na kuondolea Kampuni na washiriki wake wa mradi, kwa kiwango kinachoruhusiwa kisheria, dhima yoyote ambayo huenda wakapata kwa pamoja au mara kwa mara kuhusiana na madai, mashtaka au hatua za kisheria, zinazotokana na ushiriki wako katika Mradi.

Kazi katika Mradi huu huenda ikawa ya muda mrefu, itakayodumu kwa miaka mingi. Hati hii inatumika kwa shughuli zozote za Earthwatch ambazo utashiriki kwa kipindi hicho. Una uhuru wa kufuta kibali chako kwa kuwasiliana nasi (kupitia kwa taarifa zilizoko hapa chini) wakati wowote.

Unaweza kupakua hati hii ya kusamehe dhima sasa au baadaye kutoka kwa sehemu ya chini kwenye tovuti ya [FreshWater Watch](#)